

# **HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**



**ZABUNI NAMBA: LGA/079/2021-22/HQ/NCS/41**

## **TANGAZO LA ZABUNI**

**TAREHE: 12/06/2022**

### **UTUNZAJI WA BUSTANI PAMOJA NA MIZUNGUKO YA BARABARA MBALIMBALI KATIKA MANISPAA YA MOROGORO**

Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inakusudia kubinafsisha huduma ya utunzaji wa bustani pamoja na mizunguko ya barabara mbalimbali katika Manispaa ya Morogoro kwa mwaka wa Fedha **2022/2023**.

Eneo la huduma litakuwa katika maeneo yafuatayo;

#### **A. Bustani;**

- i. Makaburi ya wahanga wa ajali ya moto katika makaburi ya Kola
- ii. Kuzunguka majengo ya Manispaa
- iii. Mbele ya ofisi za Bima
- iv. Bustani ya Sabasaba
- v. Mbele ya Benki ya CRDB Masika
- vi. Mwere karibu na ofisi za Manispaa

#### **B. Mizunguko ya barabara (Round about):**

- i. Tumbaku
- ii. Masika
- iii. SUA
- iv. Posta
- v. Kitope karibu na ofisi ya Mkuu wa wilaya
- vi. Msamvu
- vii. Katikati ya mji karibu na stendi ya zamani ya daladala

#### **ZINGATIA:**

Kazi zitakazofanywa na mtoa huduma (MH) ni, kumwagilia maji kila siku, kungolewa nyasi kwa mikono, kupruni, kupuliziwa madawa ya kuua wadudu na kuzuia magonjwa, kutoa nyasi maua na miti iliyoaribika au kudhoofika na kupanda mingine, na kila baada ya miezi sita kufanya maboresho ya kung'oa na kupanda upya maua au nyasi.

Zabuni hii itaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 7 (2011) na Kanuni zake za mwaka 2013, Tangazo la Serikali Na. 446 na marekebisho ya kanuni ya mwaka 2016

**Sifa za mwombaji:-**

- i. Ambatanisha kivuli cha VAT.
- ii. Nakala ya usajili wa mlipa kodi TIN (kwa makampuni).
- iii. Nakala ya hati ya usajili wa kampuni.
- iv. Mwombaji lazima aambatanishe TAMKO RASMI LA VITENDO DHIDI YA KUZUIA RUSHWA iliyosainiwa na mwombaji mwenyewe.
- v. Kampuni lazima iwe imesajiliwa na kupewa leseni ya Usafi.
- vi. Kamati ya tathimini itakagua ofisi pamoja na vitendea kazi vyote vinavyo milikiwa na kampuni husika
- vii. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe **16/06/2022** saa **4:00** asubuhi na ndiyo siku ya ufunguzi wa zabuni hii.

Mwisho wa kupokea Zabuni ni saa nne (**6:00**) asubuhi siku ya Alhamisi tarehe **16/06/2022** na mara baada ya hapo Zabuni zitafunguliwa kupitia mfumo wa Ununuzi kwa njia ya Kielektroniki (**TANePS**)

Ally Machela  
MKURUGENZI WA MANISPAA  
**MOROGORO**